**MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)**

**NAMBA YA MALALAMIKO: GA.71/135/LZ/2025/01**
**NAMBA YA LOIS: COMP-2025-00000013**

**KATI YA**

**OBADIA ATHANAS POPO ............................................................ MLALAMIKAJI**

**NA**

**SHIRIKA LA UMEME TANZANIA ............................................. MLALAMIKIWA**

---

**AMRI**

---

***(Imetolewa na Katibu wa Bodi ya Wakurugenzi ya EWURA tarehe 28 mwezi wa Februari 2025)***

**MALALAMIKO HAYA** yameletwa mbele ya Katibu wa Bodi ya Wakurugenzi ya EWURA kwa ajili ya kutoa uamuzi leo tarehe 28 mwezi Februari 2025, kwa madai kwamba Mlalamikiwa ahamishe akaunti ya Mlalamikaji kutoka kwenye kundi la kati la watumiaji wa umeme T1 kwenda kwenye kundi la watumiaji wadogo wa umeme D1 kwa kuwa matumizi ya umeme ya Mlalamikaji ni chini ya uniti 75 kwa mwezi.

Baada ya kupokea malalamiko hayo, mnamo tarehe 9 Januari 2024, Mamlaka (EWURA) ilimwandikia Mlalamikiwa na kumuamuru kuwasilisha utetezi wake kwa maandishi ndani ya siku ishirini na moja (21) kwa mujibu wa Kanuni ya 6 (1) na 7 (1)

ya Kanuni za EWURA za Utatuzi wa Migogoro - (*EWURA (Consumer Complaints Settlement Procedure), Rules 2020*)).

Mnamo tarehe 10 Februari 2025, Mlalamikiwa aliwasilisha utetezi wake na kukiri kupokea malalamiko ya Mlalamikaji na kuifahamisha Mamlaka kwamba amekwisha badilisha akaunti ya Mlalamikaji kwenda kwenye kundi la watumiaji wadogo wa umeme D1 kama alivyoomba. Baada ya kupokea majibu kutoka kwa Mlalamikiwa Mamlaka ilimtafuta Mlalamikaji ili kuthibitisha kama majibu ya Mlalamikiwa ni ya kweli lakini hakupatikana. Baada ya hapo Mamlaka ilipanga kikao cha usuluhishi tarehe 12 Februari 2024 ambapo Mlalamikaji alifika na kuthibitisha ni kweli amekwishahamishiwa kwenye kundi la watumiaji wadogo wa umeme D1. Vilevile, tarehe 14 Februari 2024, Mlalamikaji alileta barua ya kuomba kuondoa malalamiko yake sababu yamekwishafanyiwa kazi. Hivyo basi, Mlalamikaji anaomba kuondoa shauri lake EWURA.

Katibu wa Bodi **ANATOA AMRI** kwamba malalamiko haya yanaondolewa na kila upande utabeba gharama za uendeshaji wa malalamiko haya.

**IMETOLEWA KWA LAKIRI** ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) hapa Dodoma leo tarehe 28 mwezi Februari 2025.

..............................
**TONI S. MBILINYI**
**KATIBU WA BODI**